Raiamwema, August 13-19 PG3

# Bodaboda, bajaji jino nje

**Na Mwandishi Wetu, Moshi**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imetekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kurasimisha shughuli za 'maofisa usafirishaji' wa pikipiki 'bodaboda' na 'bajaji'.

Hayo yalisemwa jana na Mtendaji Mkuu wa LATRA, CPA Habibu Suluo kwenye hafla ya utoaji vyeti kwa wasafirishaji kupitia bodaboda na bajaji mkoani Kilimanjaro, waliohitimu mafunzo ya udereva, iliyofanyika wilayani hapa.

"Moja ya majukumu makubwa tuliyopewa na Rais Samia wakati aliponiteua miaka mitatu iliyopita, ni kuhakikisha LATRA inarasimisha usafirishaji wa bodaboda na bajaji, ili kuboresha maisha ya wanaofanya shughuli hizo," alisema.

Alisema kwa kuanzia, LATRA ilianza mpango wa kuhakikisha wahudumu hao wanapa elimu rasmi ya udereva na kupata vyeti, kama walivyo wahudumu wengine wa usafirishaji.

"Tulishirikiana na Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA), na tayari baadhi ya waendesha bodaboda na bajaji wamehitimu na kupata leseni za udereva," alisema.

Alisema pia LATRA ilishirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, (MoCU) kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya ushirika, wahudumu hao ili wapate welewa wa kuweka akiba.

Pia uendeshaji vyama vya ushirika na jinsi ya kutumia mikopo kwa ajili ya kuboresha shughuli zao na maisha yao kwa ujumla.


"Mafunzo haya yaliwezesha kuanzishwa kwa Chama cha Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa waendeshaji hao mkoani Kilimanjaro (KIBABOT Saccos); chama hiki kimechangia kuboresha shughuli, maisha yao na ya familia zao.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa maono yake ambayo mbali na kuboresha maisha na shughuli za wanachama wa KIBABOT, pia yamechangia kupanua wigo wa huduma za LATRA kwa kiasi kikubwa," alisema.

Alisema KIBABOT ni Saccos ya kwanza kuanzishwa na wahudumu wa

CamScanner

Nipashe Jumatano 13 Ag PG 9.




# Idadi abiria wanaosafiri kwa mabasi hadharani

**Na Godfrey Mushi,**
MOSHI

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, amesema wana takwimu za abiria wote wanaosafiri kwa siku nchini kwa kukata tiketi za kielektroniki na miamala ya nauli zinazolipwa.

Suluo, aliyasema hayo jana mjini hapa wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti kwa waendesha pikipiki 178 na pikipiki kwa wanachama wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Bajaji na Bodaboda, Mkoa wa Kilimanjaro (KIBABOT).

"Kwa sasa tulipofikia, tunaweza kufahamu abiria wanaosafiri kwa siku, ambao wamekata tiketi kwa kutumia njia ya kielektroniki. Ninaweza nikakupa hesabu ya jana, mfano kwenye simu yangu," alisema na kuongeza kuwa:

"Kila siku asubuhi naweza nikapata taarifa ya abiria wote na majina yao waliosafiri nchini, miamala iliyofanyika . Ndio maana tunasema tumeithibitisha mifumo, na sisi hatutoi leseni kwa wale wanaokatisha tiketi, kwa sababu taarifa zile ni za siri, zisije zikadukuliwa."

Kuhusu bodaboda na bajaji, Suluo, alisema ni eneo la kipekee linalohitaji ' watu kujisimamia wenyewe,kuweka nidhamu na kuwa kwenye umoja kwa maana ya Chama cha Ushirika.

Alisema hayo ni moja ya mapendekezo yao, kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Godfrey Mnzava, alisema kupata mafunzo ni hatua moja na kuishi katika mafunzo ni nyingine.

Mnzava, alitoa rai kwa vijana hao kutumia mafunzo waliyoyapata katika Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) Moshi kuendana na dhamira nzuri ya serikali ya kujiajiri.

"Niwapongeze kwa kuchangamkia fursa hii iliyoletwa na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupunguza kiasi kikubwa cha gharama za utoaji wa mafunzo ya udereva na utoaji leseni," alisema afanua Mkuu huyo wa Wilaya,.



Ofisa Ushirikishwaji Jamii wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Tanga, Joseph Ng'eve, akizungumza wakati akitoa elimu kuhusu matatizo ya afya ya akili kutokana na msongo wa mawazo na kuchukua maamuzi mabaya katika Kituo cha Polisi cha Mang'enya, wilayani Muheza. Wengine ni Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, Charles Ntenga (wa tatu kulia) na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa wilaya hiyo, Leonard Bandola. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

CamScanner

Mwananchi Jumatano Agosti 13/2025 Pg 2

# Maandalizi mwendokasi Mbagala yashika kasi

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Maandalizi ya kuanza kwa usafiri wa mabasi yaendayo haraka (BRT) awamu ya pili, katika barabara ya Mbagala (Kilwa), sasa yameanza kuchangamka.

Hii ni baada ya kupita wiki moja tangu mabasi 99 kati ya 250 yatakayotumika katika awamu ya kwanza kutoa huduma, kuingia jijini Dar es Salaam yakitokea nchini China yalikotengenezwa.

Mabasi hayo, mali ya Kampuni ya Mofat, ni sehemu ya mabasi 250 yatakayotoa huduma katika njia hiyo, ikiwa ni utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo.

Barabara ya Mbagala yenye urefu wa kilomita 20.3 kutoka Mbagala hadi Gerezani, ilijengwa na Kampuni ya Sinohydro kutoka China na ilikabidhiwa kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart) tangu Agosti 2023.

Katika awamu hiyo, kampuni hiyo ndiyo imepewa mkataba wa miaka 12 kutoa huduma hiyo na mabasi yake yatatumia nishati ya gesi asilia barabara hiyo inayohitaji jumla ya mabasi 755.

Hata hivyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart), Dk Athuman *Kihamia aliimbia Mwananchi hivi karibuni kuwa, mabasi hayo kuanza kutoa huduma ni ndani ya mwezi huu (Agosti), kutokana na wananchi kusubiria kwa muda* mrefu.



Unaweza sema ni matayarisho ya mwisho mwisho kabla ya kuanza kazi, mfanyausafi akisafisha kituo cha mabasi yaendayo haraka katika eneo la Kwa Aziz Ally jijini Dar es salaam jana. **Picha na Nasra Abdallah**

Dk Kihamia alisema licha ya ujenzi wa mageti janja kutokamilika kujengwa ambayo abiria wangeyatumia kupita kwa kutumia kadi, wameona waanze na tiketi kwa ajili ya kipindi cha mpito.

Pia, taarifa kutoka chanzo cha kuaminika, ilieleza kuwa, malengo ni kuanza kuwaingiza madereva barabarani wiki hii kama moja ya kufanya majaribio na kuizoea njia hiyo na tayari madereva 150 wamekidhi vigezo na kupitishwa kuifanya kazi hiyo.

Hata hivyo, wakati mabasi hayo yakiwa bado yamehifadhiwa Bandari ya Dar es Saalam hadi sasa, usafi umeanza kufanyika kwa kasi katika vituo.

Jana, *Mwananchi* imepita katika vituo hivyo na kushuhudia usafi ukifanyika kuanzia maeneo ya Kurasini Ufundi hadi Mbagala kukiwa na watu wanafanya usafi wakiwa na mafagio na majaba ya maji.

Wapo walioonekana wakiwa wanafuta vioo, pia, wapo walioonekana wakipiga deki na kumwaga maji ndani ya vituo hivyo.

Vilevile, vituo vyote vilionekana mageti yake kufunguliwa, mengine yakifunguliwa upande mmoja na mengine pande zote na kuwapo kwa mifuko mikubwa myeusi pembezoni mwa vituo hiyo iliyotumika kuwekea takataka.

Wakizungumza kwa masharti ya kutotajwa majina, baadhi ya wafanyausafi walisema usafi huo wameuanza leo na ni kazi ya kusafisha vituo vyote vilivyopo katika barabara hiyo.

"Kama unavyoona, tunafanya usafi kwa kuwa ukweli ni kwamba vituo vilikuwa vichafu, hata kwa nje mkipita mlikuwa mnaviona, isingekuwa rahisi watu kuanza kuvitumia bila usafi," alisema msafishaji huyo.

Ukiacha suala la usafi, pia, vizuizi vyote vilivyokuwa vimewekwa katika barabara hiyo vimeondolewa, jambo ambalo limesaidia kupunguza foleni kwa kuwa sasa magari madogo, bodaboda, bajaji na maguta yanapita katika barabara hiyo huku malori na daladala yakiendelea kutumia njia ya kawaida.

Baadhi ya madereva wanaotumia barabara hiyo wamesema hilo limetokea tangu Jumamosi na kueleza kuwa imewasaidia kuepuka foleni iliyokuwa ni kero katika barabara hiyo tangu ilipopigwa marufuku barabara hiyo kutumika.

Vilevile, *Mwananchi* ilishuhudia baadhi ya maofisa wanaosemekana ni kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) wa Dart, wawakilishi kutoka Kampuni Sinohydro iliyotengeneza miundombinu wakiwa wanafanya kaguzi katika maeneo mbalimbali.

Walionekana katika mataa ya Kamata, na wiki iliyopita *Mwananchi* iliripoti kuwapo kwa kipande cha barabara ambacho hakijamalizika kutengenezwa.

Pia, wengine walikuwapo ndani ya kituo kikubwa cha mabasi hayo Mbagala Rangi Tatu ambako mabasi hayo yataanzia safari zake na kupatumia pia kama karakana na sehemu ya kujazi gesi.

Aidha, katika Kituo cha Africab Mivinjeni, eneo ambalo mwandishi wa habari hizi wiki iliyopita alishuhudia nguzo mbili za taa za kuongozea magari zilikuwa zimedondoka maeneo hayo baada ya kugongwa na gari, tayari zimeondolewa.

Wakitoa maoni yao katika hilo, baadhi ya wananchi akiwamo Dyana George, mkazi wa Mtoni, alisema sasa wanaona kweli mambo yanaenda kuanza.

"Kama na usafi wameanza kufanya, kweli mambo yameiva kwa kuwa tuna imani hawawezi tena kupaacha pachafuke ndio waweke mabasi barabarani," alisema Dyana.

Meshack Lucas, mkazi wa Kijichi alisema pamoja na hilo lililofanyika, bado haamini mpaka pale atakapoona mabasi hayo barabarani na yakiwa yameanza kutoa huduma kwa abiria.

CamScanner

Uhuru 13 Agosti /2025 Pg 19

# Sababu dereva kufungiwa leseni yake miezi mitatu

KIDAWA MOHAMED Na FLORAH PROJESTUS (UDSM)

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, imemhukumu Mazoea Musa (34), kulipa faini ya sh. 15,000 au kutumikia kifungo cha mwaka mmoja gerezani, baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kuendesha chombo cha moto kwa uzembe.

Pia, mahakama iliamuru Musa, mkazi wa Tabata Segerea, kufungiwa leseni yake ya udereva kwa muda wa miezi mitatu.

Hukumu hiyo ilitolewa mahakamani hapo, juzi na Hakimu Mwandamizi, Veneranda Kaseko, baada ya mshitakiwa kukiri kosa la kuendesha chombo cha moto kwa uzembe na kusababisha kushindwa kukizuia, hivyo kuharibu wa chombo kingine.

"Mshitakiwa umesomewa shtaka umekiri, pia umekubali mahakama ipokee vielelezo bila ya pingamizi, hivyo imekutia hatiani na kutakiwa kulipa faini ya shilingi 15 au kutumikia kifungo cha mwaka mmoja gerezani. Pili, leseni ya udereva inafungiwa kwa miezi mitatu," alisema.

Hakimu Kaseko alivitaja vielelezo ambavyo mahakama imevipokea ni maelezo ya onyo ya mshitakiwa kutoka kwa polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, ramani ya tukio na leseni ya udereva ya mshitakiwa.

Awali, Wakili wa Serikali, Dickson Swai aliiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshitakiwa iwe fundisho kwake na kwa wengine kwa kuwa makosa hayo yanazidi hivi sasa.

Mshitakiwa alitenda kosa Februari 19, mwaka huu, Magomeni Kagera, Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam, ambapo aliendesha gari aina ya Mercedes Benz lenye namba T363 EGE kwa uzembe na kushindwa kulizuia hivyo kuligonga gari aina ya ZHONGTONG lenye namba T328 DUS.

CS CamScanner

Zanzibar Leo



# Ajali ya gari yaua watu 10 Peru

**LIMA, PERU**

TAKRIBAN watu 10 wameuawa na wengine 37 kujeruhiwa kusini mwa Peru wakati basi la abiria lilipotumbukia umbali wa mita 200 kwenye bonde katika eneo la Sandia, mkoa wa Puno, polisi wa eneo hilo walisema.

Basi hilo lilikuwa likisafiri kutoka jiji la Juliaca kuelekea San Pedro de Putina Punco wakati lilipotumbukia kwenye mto Inambari.

Polisi wa eneo hilo waliwaokoa abiria 37 waliokuwa wamekwama kwenye mabaki ya gari hilo, ambao baadaye walipelekwa katika hospitali ya karibu kwa matibabu.

Chanzo cha ajali hiyo bado kinachunguzwa.

Ajali za barabarani ni za kawaida nchini Peru, mara nyingi huhusishwa na hali mbaya ya barabara na magari yaliyochakaa, pamoja na mazoea hatari kama vile kuendesha gari bila leseni na ulevi.

CamScanner

Zanzibar leo Jumatano 13 August, PG 18

# LATRA yarasimisha usafiri pikipiki, bajaji

NA KIJA ELIAS, MOSHI

**MAMLAKA ya Usafiri wa Ardhini (LATRA) imefanikiwa kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, lililoitaka kurasimisha shughuli za usafirishaji kupitia pikipiki na bajaji.**

Hayo yalisemwa jana na Mtendaji Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, wakati wa hafla ya kuwatunuku vyeti wahudumu wa bodaboda na bajaji waliohitimu mafunzo ya udereva mkoani Kilimanjaro, iliyofanyika katika wilaya ya Moshi.

"Moja ya majukumu niliyopewa na Rais Samia aliponiteua miaka mitatu iliyopita ni kuhakikisha LATRA inarasimisha shughuli za usafirishaji kwa kutumia bodaboda na bajaji ili kuimarisha maisha ya wahudumu hao," alisema Suluo.

Alieleza LATRA ilianza kwa kuhakikisha wahudumu hao wanapata elimu rasmi ya udereva kupitia ushirikiano na Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA), hatua iliyowezesha wengi kupata vyeti na leseni rasmi za udereva.

"Tulishirikiana na VETA kuwapa mafunzo ya udereva na tayari baadhi yao wamehitimu na kupata leseni. Pia tulishirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kuwapatia elimu ya ujasiriamali na ushirika," alieleza.

Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo katika kuweka akiba, kuendesha vyama vya ushirika, pamoja na matumizi sahihi ya mikopo ili kuboresha maisha yao na shughuli zao za kila siku.

"Kupitia mafunzo haya, tumeweza kuanzisha Chama cha Akiba na Mikopo cha waendesha bodaboda na bajaj mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS), ambacho kimeleta mabadiliko chanya katika maisha ya wahudumu hawa na familia zao," aliongeza.

Alisema KIBABOT SACCOS ni chama cha kwanza cha ushirika kilichoanzishwa na waendesha bodaboda nchini, na mafanikio yake yameanza kuenea katika mikoa mingine kama Mwanza na Dar es Salaam.

"Hivi karibuni, tunatarajia kuanzisha SACCOS nyingine kwa wahudumu hao jijini Dar es Salaam. Haya yote ni matokeo ya maono ya Rais Samia yanayolenga kuboresha maisha ya Watanzania wa kada zote," alisema.

Katika hafla hiyo, LATRA pia ilikabidhi pikipiki 10 kwa wanachama wa KIBABOT SACCOS kupitia mpango wa mikopo nafuu ili kuwawezesha kuboresha shughuli zao.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa KIBABOT wilaya ya Moshi, Hamad Bendera, alimshukuru Rais Samia kwa jitihada zake za kuwainua wahudumu wa usafirishaji kupitia elimu na uwezeshaji.

"Kupitia elimu tuliyopata, leseni na uanzishwaji wa chama chetu cha ushirika, sasa tunaendesha maisha yetu na ya familia zetu kwa uhakika na heshima," alisema.

Aliongeza kuwa Rais Samia alitoa maelekezo ya kupunguza gharama za mafunzo kutoka shilingi 150,000 hadi shilingi 30,000, na ada ya leseni kutoka shilingi 83,000 hadi shilingi 30,000, jambo lililowavutia wengi kujiunga na mafunzo hayo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa wilaya ya Moshi, Godfrey Mnzava, aliwataka wahitimu wa mafunzo hayo kutumia vyema elimu waliyoipata ili kupunguza ajali za barabarani.

"Natoa rai kwa wanaopata mikopo ya pikipiki kuitumia vizuri, kufanya kazi kwa bidii na kulipa mikopo kwa wakati ili wengine nao wanufaike kupitia SACCOS yenu," alisema.

Awali, Ofisa Mfawidhi wa LATRA mkoa wa Kilimanjaro, Paul Nyello, alisema wahudumu 178 wa bodaboda na bajaji wamehitimu mafunzo hayo yaliyofanikishwa kwa ushirikiano na VETA.